

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI

27 JUNI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI – TAREHE 27 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (*The Finance Bill, 2022*).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (*The Finance Bill, 2022*).

### **III. MASWALI:**

#### **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

##### **455. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Utigi hadi Kirongwe.

##### **456. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa treni ya mwendokasi kutoka Kaliva, Mpanda hadi Karema.

## **WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **457. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,  
Sanaa na Michezo:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni mabadiliko ya  
Sheria ya Hakimiliki ili iwezeshe Mkataba wa  
Marakesh kutekelezeka kwa mujibu wa Sheria.

### **458. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,  
Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mpango gani kuruhusu Watu/Taasisi  
binafsi hasa za Wasanii kukusanya mirahaba  
maeneo ya wazi yanayotumia kazi za sanaa.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **459. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINKIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na  
Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga majengo mapya ya kisasa ya Mahakama ya Wilaya Hai kwa kuwa jengo la sasa ni chakavu.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**460. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

• Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Muleba.

**461. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Chuo Kikuu cha Dodoma na Vyuo vingine ambavyo vilijengwa na kuonekana vina dosari.

## **WIZARA YA KILIMO:**

**462. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA  
KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sekta ya Kilimo inakuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**463. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN  
KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, hasara na faida gani Taifa linapata kuwa uchumi wa kati na asilimia ngapi ya Wananchi wanafahamu na kuishi uchumi wa kati.

**IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima  
na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022  
*(The Finance Bill, 2022).*



DODOMA  
27 JUNI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE